



Sensa 2020

**Wewe
ni wa thamani.
Hakikisha
unahesabiwa.**




10 dakika
maswali
miaka

Inachukua takribani dakika 10 kujibu maswali 10 ambayo yatatumika kuandaa masuala ya uwekezaji kwenye jumuiya yako kwa miaka 10.



www.ofm.wa.gov/2020census



Utapata mwaliko kupitia barua

Kila kaya itakuwa na chaguo la kushiriki kwa njia ya mtandao, kwa barua au kwa simu. Dodoso za mtandaoni na za simu zinapatikana kwa Kiingereza na kwa lugha 12 zisizo za Kiingereza.

Tarehe husika au katikati:

Utapokea kwenye sanduku la posta la nyumbani kwako:

Machi 12-20

Mwaliko wa kushiriki Sensa 2020 kwa njia ya mtandao.
(Baadhi ya kaya zitapokea pia dodoso za karatasi.)

Machi 16-24

Barua ya kukumbushwa.

Kama bado utakuwa hujashiriki:

Machi 26-Aprili 3

Kadi Maalum ya kukumbushwa.

Aprili 1

Siku ya Sensa

Aprili 8-16

Barua ya kukumbushwa na dodoso la karatasi.

Aprili 20-27

Kadi Maalum ya mwisho ya kukumbushwa kabla ya Ofisi ya Sensa ya Marekani haijatuma mtu kufuatilia.



Jihesabu mwenyewe

Pale unapoishi na unapolala mara nyingi kufikia Aprili 1, 2020.

Majibu yako ya Sensa 2020 ni salama na siri na yanalindwa kisheria.

Ofisi ya Sensa haitatoa majibu yako kwa mahakama yoyote au shirika lingine la kiserikali, ikiwemo FBI, ICE au Idara ya Ulinzi ya Marekani.

Ofisi ya Sensa **KAMWE**:

- Haitakutumia barua pepe.
- Haitakuomba nambari yako ya Huduma za Kijamii (SSN), jina la awali la mama yako, taarifa za akaunti yako ya benki, fedha, au chochote kile kwa niaba ya chama cha siasa.
- Haitakuomba kuja nyumbani kwako.
- Haitakutishia kukukamata kama hutoshirikiana nao.

www.ofm.wa.gov/2020census